# HISTORIA YA OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI KUANZIA 1961 HADI 2024

## 1.0 UTANGULIZI

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni zao la Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Majukumu ya Ofisi hii yanaelezwa katika Ibara ya 59(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, na pia Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa mwaka 2018 pamoja na Tangazo la Serikali Namba 48 la mwaka 2018.

Pamoja na majukumu mengine, Ofisi hii inawajibika kutoa ushauri kwa Wizara, Idara za Serikali na Taasisi nyingine za Serikali na Mashirika ya Umma kuhusu mchakato wa kutunga sheria na ushauri wa kisheria katika masuala ya jumla na katika uandaaji wa miswada kwa ajili ya kupitishwa na Bunge ili kuwa sheria.

## 2.0 KIPINDI CHA UTAWALA WA MWINGEREZA

Nchi ya Uingereza iliitawala Tanganyika kwa kipindi cha miaka 40 yaani kuanzia mwaka 1921–1961. Katika kipindi hiki cha utawala wa Kiingereza, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliingizwa rasmi katika Sheria kupitia Amri za Baraza la Tanganyika kufuatia marekebisho yaliyofanyika mwaka 1945. Marekebisho haya yalileta Muundo wa Baraza la Tanganyika ambalo Mwanasheria Mkuu alitajwa kuwa miongoni mwa Wajumbe wa Baraza la Tanganyika pamoja na Katibu Mkuu Kiongozi, Katibu Mkuu Hazina na Mkurugenzi wa Huduma za Afya.

Historia inaeleza zaidi kuwa, kupitia Mkataba wa Kimataifa wa Geneva wa Mwaka 1906 na 1929 (Mamlaka ya Makoloni) Amri za Mabaraza ya mwaka 1937, Mwanasheria Mkuu wa Serikali alikuwa ni Afisa Mkuu wa Mamlaka ya Makoloni ambaye alikuwa na jukumu la kusimamia na kutetea mashauri yaliyofunguliwa mahakamani dhidi ya Afisa wa Serikali au Mashirika hodhi katika kutekeleza majukumu waliyopewa. Kufuatia amri hiyo, mashauri yoyote hayakuweza kufunguliwa bila idhini ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

## 3.0 OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI BAADA YA UHURU

Mwaka 1961 Tanganyika ilipata Uhuru na ikaanza kujitawala yenyewe. Ingawa kabla ya Uhuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilikuwepo, Katiba ya Uhuru ilitungwa ili kuwezesha Tanganyika kujitawala. Hivyo kupitia Ibara ya 5(2) ilitamkwa kwamba Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali itaendelea kuwepo mara baada ya kuanza kwa Katiba

hiyo. Hii ilipelekea Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuendelea kuwepo ikiwa chini ya Wizara ya Sheria kufuatia Hati ya Mgawanyo wa Madaraka kupitia Tangazo la Serikali Namba 27 la mwaka 1962. Ofisi hii iliendelea kuwa chini ya Wizara hiyo hata baada ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar mwaka 1964.

Uchaguzi Mkuu wa mwaka 1965 uliambatana na mabadiliko makubwa ya kimuundo ambapo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kupitia Hati ya Mgawanyo wa Madaraka, Tangazo la Serikali Namba 104 la mwaka 1966, iliwekwa chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Ofisi hii iliendelea kuwa chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais hadi Mwaka 1970 ambapo baada ya Uchaguzi Mkuu kupitia Hati ya Mgawanyo wa Madaraka Tangazo la Serikali Namba 285 la Mwaka 1972, iliwekwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais kama ilivyokuwa wakati huo.

Baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 1975, kupitia Tangazo la Serikali Na 10 la Mwaka 1976 Wizara ya Sheria iliundwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilirudishwa Wizara ya Sheria kutokea Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Pili wa Rais. Katika kipindi hiki pia Serikali ilianza kutekeleza mpango wake wa kusogeza huduma ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika ngazi ya kanda ambazo ni Mwanza, Arusha, Tabora, Dodoma, Mbeya na Mtwara. Mwaka 1983 yalifanyika mabadiliko madogo katika Muundo wa Serikali ambapo aliyekuwa Mwanasheria Mkuu pia alikuwa Waziri wa Sheria; Utaratibu huu uliendelea hata baada ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 1985. Hata hivyo, Mabadiliko makubwa ya Baraza la Mawaziri yaliyofanywa mwaka 1990 yalipelekea kufutwa kwa Wizara ya Sheria na hivyo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilirudishwa tena Ofisi ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais kupitia Tangazo la Serikali Na. 140 la Mwaka 1990, kama Idara inayojitegemea.

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliendelea kupitia maboresho mbalimbali kwa lengo la kuiimarisha kimfumo na kiutendaji. Mabadiliko ya Tano ya Katiba yaliitambua rasmi Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na mamlaka yake. Utendaji na majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali yaliendelea kuboreshwa kufuatia kutungwa kwa Sheria ya mwaka 1991 ambayo iliwezesha ushirikiano kati ya Tanzania na Nchi za Jumuiya ya Madola au nchi nyingine kwenye masuala ya jinai ili kusaidiana katika kushughukikia uhalifu wa kijinai. Aidha, katika kipindi hili zilifunguliwa Ofisi za Kanda za Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika Mikoa ya Tanga, Ruvuma, Kilimanjaro, Dar es Salaam, Kagera na Rukwa na kufanya jumla ya Ofisi za Kanda kuwa kumi na mbili.

Mafanikio makubwa yaliyopatikana ni uimarishaji wa Ofisi za Kanda zilizokuwepo na kuwajengea uwezo watendaji katika Sekta ya Sheria kitaaluma na kiutendaji.

Pia Divisheni ya Haki za Binadamu na Mambo ya Katiba katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilianzishwa mwaka 1998. Divisheni hii ilishughulikia pamoja na mambo mengine masuala ya Katiba na Haki za Binadamu. Vile vile taarifa za utekelezaji wa haki za Binadamu ziliwasilishwa katika Kamati ya Kamisheni ya Haki za Binadamu inayosimamia utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa dhidi ya Ubaguzi wa Rangi. Maboresho haya yalisaidia kuboresha upatikanaji wa huduma bora za kisheria kwa wakati ili wananchi watumie muda mfupi kupata haki zao na hivyo kujikita katika shughuli zao za kiuchumi.

## 4.0 MUUNDO WA OFISI YA MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI

Baada ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 1995, Wizara Mpya ya Sheria na Mambo ya Katiba iliundwa kupitia Tangazo la Serikali Namba 720 la Mwaka 1995. Katika Muundo huo, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilikuwa chini ya Wizara ya Sheria na Mambo ya Katiba. Pamoja na mabadiliko yote yaliyokuwa yanafanyika, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliendelea kutekeleza majukumu yake ya kuwa Mshauri Mkuu wa Serikali katika masuala yote ya Kisheria, hususani Uendeshaji wa Mashtaka, Madai na Mikataba ya Kimataifa, Kabidhi Wasii na Uandishi wa Miswada ya Sheria. Ofisi hii wakati huo iliundwa na Divisheni nne ambazo ni:

*(a)* Divisheni ya Uendeshaji wa Mashtaka;

*(b)* Divisheni ya Uandishi wa Sheria;

*(c)* Divisheni ya Madai na Mashauriano ya Kimataifa; na

*(d)* Divisheni ya Kabidhi Wasii Mkuu wa Serikali.

Divisheni nne ziliendelea kuwepo hadi mwaka 1998 ilipoundwa Divisheni ya Katiba na Haki za Binadamu na hivyo kuzifanya kuwa tano. Baadaye Ofisi iliendelea kukua kwa kuongezeka na kuzaliwa Divisheni za Mipango na Utawala na Rasilimali Watu. Muundo uliopitishwa mwaka 2008, uliifanya Ofisi kuwa Taasisi huru kiutendaji chini ya Wizara hiyo ambapo kwa mujibu wa Muundo huo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilikuwa na Divisheni sita na vitengo saba pamoja na Ofisi za Kanda kama ifuatavyo:

(a) Divisheni:

*(i)* Divisheni ya Uendeshaji wa Mashtaka;

*(ii)* Divisheni ya Uandishi wa Sheria;
*(iii)* Divisheni ya Madai na Mashauriano ya Kimataifa;

*(iv)* Divisheni ya Katiba na Haki za Binadamu;

*(v)* Divisheni ya Mipango na Sera; na *(vi)* Divisheni ya Utawala na Rasilimali Watu.

*(b) Vitengo:*

*(i)* Kitengo cha Ununuzi na Ugavi;

*(ii)* Kitengo cha Masjala ya Sheria;

*(iii)* Kitengo cha Uchambuzi na Mifumo ya Kompyuta;

*(iv)* Kitengo cha Habari, Elimu na Mawasiliano;

*(v)* Kitengo cha Utafiti na Maktaba;

*(vi)* Kitengo cha Uhasibu; na

*(vii)* Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani.

Muundo huu uliendelea kuboreshwa hadi kufikia mwaka 2018 ambapo mabadiliko makubwa yalifanyika baada ya kugawanywa kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika Ofisi tatu zinazojitegemea chini ya Wizara ya Katiba na Sheria ambazo ni Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. Mabadiliko haya yalisababisha kufanyika marekebisho katika Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kutungwa kwa Muundo mpya wa mwaka 2018 ambao umepelekea kuwepo na Divisheni tano na vitengo sita kama ifuatavyo:

*(a)* Divisheni

*(i)* Divisheni ya Uandishi wa Sheria;

*(ii)* Divisheni ya Mikataba na Makubaliano ya Kimataifa;

*(iii)* Divisheni ya Uratibu na Huduma za Ushauri;

*(iv)* Divisheni ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu; na
*(v)* Divisheni ya Mipango.

*(b)* Vitengo

*(i)* Kitengo cha Huduma za Maktaba na Utafiti;

*(ii)* Kitengo cha Fedha na Uhasibu;

*(iii)* Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani;

*(iv)* Kitengo cha Usimamizi wa Ununuzi;

*(v)* Kitengo cha TEHAMA; na

*(vi)* Kitengo cha Mawasiliano Serikalini.

## 5.0 HALI YA UONGOZI

Hadi kufikia sasa, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imekuwa na Wanasheria Wakuu wa Serikali kumi na katika nafasi ya Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni Ishirini. Mchanganuo wa hali ya Uongozi wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali unaonekana katika majedwali yanayofutayo:

Jedwali Na. 1: **Orodha ya Wanasheria Wakuu wa Serikali 1961 – 2023**

| Na. | Jina | Mwaka |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Roland Brown | 1964 – 1965 |
| 2. | Mhe. Mark Bomani | 1965 – 1976 |
| 3. | Mhe. Jaji Joseph S. Warioba | 1976 – 1985 |
| 4. | Mhe. Damian Z. Lubuva | 1985 – 1993 |
| 5. | Mhe. Andrew J. Chenge | 1993 – 2005 |
| 6. | Mhe. Johnson P. J. Mwanyika | 2005 – 2009 |
| 7. | Mhe. Jaji Frederick M. Werema | 2009 – 2014 |

| | | |
|---|---|---|
| 8. | Mhe. George M. Masaju | 2015 – 2018 |
| 9 | Mhe. Prof. Adelardus L. Kilangi | 2018 – 2021 |
| 10 | Mhe. Dkt. Eliezer M. Feleshi | 2021- 2024 |
| 11 | Mhe. Hamza Johari | 2024- |

Jedwali 2: **Orodha ya Manaibu Wanasheria Wakuu wa Serikali 1961 - 2023**

| Na. | Jina | Mwaka | Cheo |
|---|---|---|---|
| 1. | David Levric Davies,O.B.E | 1961 – 1963 | Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Solicitor General) |
| 2. | Mhe. Mark D. Bomani | 1963 – 1965 | Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali (Solicitor General) |
| 3. | Mhe. Bob Makani | 1965 – 1965 | Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali |
| 4. | Arnold Kileo | 1965 – 1976 | Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali |
| 5. | Damian Z. Lubuva | 1976 – 1977 | Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali |
| 6. | George Liundi | 1977-1977 | Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali |
| 7. | Damian S. Meela | 1977-1987 | Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali |
| 8. | T.L. Mkude | 1987-1991 | Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali |
| 9. | Andrew Chenge | 1991-1993 | Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 10. | Felix Mrema | 1993-1997 | Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali |
| 11. | Kulwa Masaba | 1997-2002 | Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali |
| 12. | Johnson P.M. Mwanyika | 2002-2005 | Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali |
| 13. | Vicent D.K. Lyimo | 2005-2008 | Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali |
| 14. | Sazi B. Salula | 2008-2009 | Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali |
| 15. | George M. Masaju | 2009-2015 | Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali |
| 16. | Dkt Tulia Ackson | 2015-2015 | Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali |
| 17. | Gerson J. Mdemu | 2016-2018 | Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali |
| 18. | Paul J. Ngwembe | 2018-2018 | Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali |
| 19. | Dkt. Evaristo K. Longopa | 2018-2023 | Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali |
| 20. | Balozi Prof. Kennedy G. Gastorn | 2023- 2024 | Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali |
| 21 | Samwel Maneno | 2024- | Naibu Mwanasheria Mkuu wa Serikali |

## 6.0 MAJUKUMU

Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali yameainishwa katika Ibara ya 59(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1997, Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura ya 268 na Muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali wa Mwaka 2018, Tangazo la Serikali Na. 48 la 2008.
Majukumu hayo ni; kutoa ushauri kwa Wizara, Idara za Serikali na taasisi nyingine za Serikali na Mashirika ya Umma kuhusiana na mchakato wa kutunga sheria na ushauri wa kisheria katika masuala ya jumla; kuandaa miswada kwa ajili ya kupitishwa na Bunge kuwa Sheria; kuandaa hati zote za kisheria na maazimio kwa ajili ya kuidhinishwa na Bunge; kushauri katika usahihi na dhamira ya Sheria za Bunge, Sheria Ndogo na hati nyingine za kisheria; kuishauri Serikali katika masuala yote ya kimikataba ikijumuisha makubaliano ya kimataifa na mikataba ambayo Serikali inahusika au ina maslahi; kushauri na kudumisha ushirikiano na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa ajili ya utaratibu mzuri na wenye ufanisi wa kushughulikia mashauri yaliyofunguliwa mahakamani na kwenye mabaraza; kupokea na kutoa ushauri katika ripoti zilizowasilishwa na Wakili Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa ajili ya kuishauri Serikali, Bunge na Mahakama; kuwasimamia Maafisa Sheria na Mawakili wa Serikali walioajiriwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Wizara, Idara za Serikali, wakala za Serikali na Mamlaka za Serikali za Mitaa; kuwasimamia watumishi walioajiriwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; kumwita afisa yeyote wa umma kutoa maelezo, au taarifa kuhusiana na jambo lolote linakohusiana na ushauri unaotolewa; kuandaa na kuwasilisha ripoti za mwaka kwa Waziri; kuajiri na kusimamia nidhamu ya Mawakili na Maafisa wengine wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali; na kufanya kazi yoyote muhimu kwa utekelezaji wenye ufanisi wa majukumu ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

## 7.0 MATUKIO MAKUU

Kugawanywa kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika ofisi tatu zinazojitegemea chini ya Wizara ya Katiba na Sheria mwaka 2018 ambazo ni Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa Tangazo la Serikali Na. 48 la mwaka 2018, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa Tangazo Na. 49 la mwaka 2018 na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa Tangazo la Serikali Na. 50 la mwaka 2018, ni mabadiliko makubwa ya kimuundo yaliyofanyika katika ofisi hii. Mabadiliko haya yaliambatana na marekebisho makubwa ya Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura ya 268 yaliyofanywa na Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na.

2), Sheria Na. 7 ya mwaka 2018.

## 8.0 MAFANIKIO

Mafanikio ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali yanaweza kuainishwa katika awamu sita zifuatazo:

### 8.1 Awamu ya Kwanza 1961 - 1985

Katika Awamu ya Kwanza mafanikio makubwa ambayo Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliweza kuajiri Mawakili wengi wa Serikali kutokana na jitihada za Serikali za kuanzisha Kitivo cha Sheria cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ambacho kililenga kutoa mafunzo ya Taaluma ya Sheria. Lengo lilikuwa ni kupata wataalamu wa sheria ambao ni wazalendo. Kwa ujumla katika Awamu hii, wazo la kupeleka huduma karibu na Wananchi ili huduma iwafikie katika wakati muafaka lilianza kutekelezwa kwa kufungua Ofisi za Kanda za Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Kanda za mwanzo kufunguliwa ni Mwanza, Arusha, Tabora, Dodoma, Mbeya na Mtwara. Ofisi hizi za Kanda zilifunguliwa katika kipindi cha mwaka 1970-1975.

### 8.2 Awamu ya Pili 1985 - 1995

Katika Awamu ya Pili zilifunguliwa Ofisi za Kanda za Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika Mikoa ya Tanga, Ruvuma na Kilimanjaro ambapo Ofisi za kanda ziliendelea kuongezeka hadi kufikia tisa (9). Katika Awamu hii mafanikio makubwa yaliyopatikana ni uimarishaji wa Ofisi za Kanda zilizokuwepo na kujenga uwezo wa watendaji katika Sekta ya Sheria kitaaluma na kiutendaji.

### 8.3 Awamu ya Tatu 1995 - 2005

Katika Awamu ya Tatu ufunguzi wa Ofisi za Kanda za Mwanasheria Mkuu wa Serikali za Dar es Salaam, Bukoba na Sumbawanga na kufanya jumla ya Ofisi za Kanda kuwa kuwa kumi na mbili (12). Maandalilizi ya kutenganisha shughuli za uendeshaji wa Mashtaka na upelelezi yalianza. Katika kipindi hiki cha Serikali ya Awamu ya tatu, Divisheni ya Haki za Binadamu na Mambo ya Katiba katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilianzishwa mwaka 1998. Divisheni hii ilikuwa inashughulikia pamoja na mambo mengine masuala ya Katiba na Haki za Binadamu. Vile vile taarifa za utekelezaji wa haki za Binadamu zilikuwa zikiwasilishwa katika Kamati ya Kamisheni ya Haki za Binadamu inayosimamia utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa dhidi ya Ubaguzi wa Rangi. Katika kipindi hicho cha Serikali ya Awamu ya Tatu, Miswada ya Sheria ya Mabadiliko ya kumi na nne (14) ya

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Sheria ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliandaliwa.

Kutungwa kwa Sheria ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali *(The Office of the Attorney General (Discharge of Duties) Act, No. 4 ya mwaka 2005)* ilitokana na kuimarishwa zaidi katika Katiba majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ambapo Ibara ya 59(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inatoa jukumu la jumla la Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwamba "atakuwa ndiye mshauri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano juu ya mambo ya Sheria".

**8.4 Awamu ya Nne 2005 - 2015**

Serikali ya Awamu ya Nne iliboresha upatikanaji wa huduma bora za Kisheria kwa wakati ili Wananchi watumie muda mfupi kupata haki zao na hivyo kujikita katika shughuli zao za kiuchumi. Katika awamu hii, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali iliendelea kutekeleza Mpango Maalum wa kutenganisha shughuli za mashtaka na upelelezi ambazo zilikuwa zinafanywa na jeshi la Polisi. Mpango huu ulisaidia kuwa na Ofisi za Kanda katika kila mkoa. Aidha, mikakati bado iliendelea kuhakikisha huduma hiz0 zinafika hadi ngazi za Wilaya. Ofisi iliweza kuanzisha Ofisi katika mikoa ya Shinyanga, Mara, Singida, Lindi na Iringa ambazo zilifanya jumla ya Ofisi za Kanda za Mwanasheria Mkuu wa Serikali kufikia 17 katika ngazi ya mikoa. Katika utekelezaji wa mpango huu Mawakili wa Serikali zaidi ya 250 walipata ajira na kupangiwa vituo vya kazi katika Ofisi za Kanda za Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuendelea na shughuli za uendeshaji wa Mashtaka.

**8.5 Awamu ya Tano, 2015 – Machi, 2021**

Matukio muhimu yaliyotokea katika kipindi hiki ambayo yanaihusu Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni pamoja na kugawanywa kwa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali katika ofisi tatu zinazojitegemea chini ya Wizara ya Katiba na Sheria mwaka 2018 ambazo ni Ofisi ya Mwnasheria Mkuu wa Serikali kwa Tangazo la Serikali Na. 48 la mwaka 2018, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa Tangazo Na. 49 la mwaka 2018 na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa Tangazo la Serikali Na. 50 la mwaka 2018. Mabadiliko haya yaliambatana na marekebisho makubwa ya Sheria ya Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Sura ya 268 yaliyofanywa na Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Na. 2), Sheria Na. 7 ya mwaka 2018

### 8.6 Awamu ya Sita, Machi 2021 – Hadi sasa

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeendelea kuboresha utoaji huduma za kisheria na utoaji wa ushauri wa kisheria kwa lengo la kukabiliana na mabadiliko ya kimazingira, kiuchumi, kibiashara na maendeleo ya sayansi na teknolojia katika maeneo ya Uandishi wa Sheria, Urekebu wa Sheria, Ufasiri Sheria, Upekuzi, na Uchambuzi wa Mikataba mbalimbali ya kiuwekezaji. Aidha, Ofisi inaiwakilisha Serikali kitaifa, kikanda na kimataifa katika masuala yenye maslahi kwa Taifa. Huduma za kisheria ni moja ya nyenzo muhimu katika kuhakikisha Taifa linakuwa na utawala unaozingatia sheria, uwazi na uwajibikaji ili kutoa huduma bora kwa wananchi na kuendana na kipaumbele kikuu cha kujenga uchumi wa viwanda. Mafanikio yaliyopatikana ni kama yafuatayo

## 9.0 HITIMISHO:

Kwa sasa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali inaendelea na ujenzi wa mfumo wa kieletroniki (OAGMIS) na miundombinu yake kwa lengo la kuimarisha utunzaji wa taarifa za kiutawala, mikataba, utoaji wa ushauri wa kisheria, orodha ya Mawakili wa Serikali, kutunza nyaraka, habari, miongozo inayotolewa na masuala mbalimbali ya kisheria na kuendelea kuwajengea uwezo Mawakili wa Serikali. Aidha, Ofisi ina mpango wa kuanzisha Chuo cha Mafunzo ya nadharia na vitendo kwa ajili ya kuwajengea uwezo Mawakili wote wa Serikali katika maeneo mbalimbali.